**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**610** **UALIMU**

**Muda: saa 3** **Mwaka: 2019**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B, C, D** na **E** zenye jumla ya maswali **kumi na nane (18).**
2. Jibu Maswali yote katika sehemu **A** na swali **moja (1)** katika kila sehemu **B, C, D** na **E.**
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na kila sehemu **B, C, D na E** ina alama **kumi na tano (15).**
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhiswa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Fafanua hoja mbili zinazoonesha ufanano na utofauti kati ya saikolojia ya Elimu na matawi mengine ya saikolojia.
2. Haiba ni jumla ya sifa alizonazo mtu fulani zinazomfanya akubalike na watu. Taja maeneo manne ambayo sifa hizo hujitokeza.
3. (a) Eleza kwa kifipi maana ya Ujana

   (b) Eleza kwa kifupi tabia tatu zinazothibitisha uwepo wa vurugu za maono kwa kijana.
4. (a) Nini maana ya kujifunza?

   (b) Kwa kutumia hoja tatu, eleza kwa kifupi umuhimu wa kujifunza
5. Eleza kwa kifupi hoja nne kuonesha umuhimu wa azimio la kazi.
6. Orodhesha mambo manne ya kuzingatia katika kuwapanga wanafunzi kwenye vikundi vya kujifunzia katika darasa lenye wanafunzi wengi.
7. Kwa kutumia mifano, fafanua aina nne za maswali yanayohitaji majibu mafupi.
8. (a) Fasili neno "dodoso" kama linavyotumika katika utafiti.

   (b) Bainisha hatua tatu za mwanzo zinazopaswa kufuatwa wakati wa utayarishaji wa dodoso.
9. Eleza kwa kifupi maana ya vifaa vifuatavyo vya mtaala:

   (a) Media elekezi

   (b) Kiongozi cha mwalimu

   (c) Muhtasari wa somo

   (d) Kitabu cha ziada.
10. Eleza kwa kifupi mambo manne yanayoweza kuwa ni viashiria vya mtu aliyeelimika.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B ( alama 15)

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

11. Changanua sifa kuu sita anazopaswa kuwa nazo mwalimu wa unasihi katika shuke za msingi.
12. Kwa kutumia mifano, chambua sababu zinazoweza kuathiri uwezo wa mtoto katika kujifunza.

## SEHEMU C (alama 15)

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

13. Bainisha faida tatu na hasara tatu za kutumia njia ya "ziara ya kimasomo" katika ufundishaji na ujifunzaji darasani.
14. Eleza vidokezo sita muhimu vya kuzingatia katika kulimudu darasa wakati wa kufundisha na kujifunza.

## SEHEMU D (alama 15)

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

15. Fafanua aina nne za tathmini kisha toa matumizi mawili ya kila tathmini
16. Chunguza alama za wanafunzi walizopata katika mtihani wa Hisabati kisha jibu maswali yanayofuata.

| Mtahiniwa | A | B | C | D | E | F | G | H | I | J |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alama | 70 | 80 | 55 | 60 | 65 | 50 | 60 | 55 | 65 | 70 |

(a) Kokotoa:

(i) Wastani

(ii) Variansi

(iii) Achano sanifu

(b) Rekebisha alama walizopata watahiniwa A na H kwa kutumia kigezo cha "T"



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(c) Eleza kwa kifupi sababu ya kurekebisha alama za wanafunzi.

(d) Toa tafsiri ya achano sanifu ulilopata katika mchakato wa kurekebisha alama za wanafunzi A na H hapo juu.

**SEHEMU E ( alama 15)**

Jibu swali **moja tu** katika sehemu hii

17. Eleza kwa kina changamoto sita zinazochangia kushindwa kuanzishwa kwa wingi madarasa ya elimu jumuishi katika shule za msingi Tanzania.

18. Kwa kutumia mifano, jenga hoja kufafanua mambo matatu yanayoweza kumotisha na mambo matatu yanayoweza kumkatisha tamaa mwanafunzi mtu mzima katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org